## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MADINI







# WIZARA YA MADINI MGAWANYO WA MAJUKUMU KATIKA SEHEMU ZAKE

## SEHEMU YA UENDELEZAJI MIGODI

- Kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Sera za Madini
- Kutoa maoni kuhusu utungaji wa Sheria na anuni za madini
- Kutoa msaada kwa ajili ya uundaji wa mazingira mazuri kwa uwekezaji wa umma na binafsi katika sekta ya madini
- Kufuatilia na kusaidia shughuli za kitaalamu za taasisi zinazoshughulikia masuala ya madini
- Kukuza rasilimali za madini za tanzania kwa utafiti na uvunaji wa madini
- Kupitia upya mifumo ya kitaasisi, sheria na udhibiti katika sekta ya madini
- Kuratibu uanzishwaji, matengenezo na uhuishaji kanzidata za sekta ya madini
- Kutambua ujuzi unaohitajika kwa maendeleo ya sekta ya madini na kuwasiliana na taasisi za mafunzo zinazotoa ujuzi kuhusiana na sekta ya madini
- Kutambua vipaumbele vya kitaifa katika sekta ya madini na kujumuisha katika mfumo wa maendeleo ya uchumi wa taifa

## SEHEMU YA UONGEZAJI THAMANI WA MADINI

- Kuhamasisha na kuwezesha uwekezaji katika shughuli za uongezaji thamani madini katika mnyororo mzima wa uongezaji thamani madini;
- Kuandaa na kusimamia Sera na Sheria ya Uongezaji Thamani Madini nchini; Kuratibu, kuwezesha na kufuatilia minada ya kitaifa na Kimataifa ya madini ya vito nchini;
- Kuwezesha uanzishwaji wa viwanda vya uongezaji thamani madini kama vile uchakataji, uchenjuaji,usafishaji, ukataji na ung'arishaji wa madini; na
- Kutoa mafunzo ya Sheria, Kanuni na Miongozo ya shughuli za uongezaji thamani madini nchini.

## SEHEMU YA UENDELEZAJI UCHIMBAJI MDOGO

- Kuhamasisha shughuli za uchimbaji na uchenjuaji kwa Wachimbaji wadogo;
- Kuratibu upatikanaji wa maeneo ya wachimbaji wadogo yenye taarifa sahihi za kijio-sayansi na kuratibu ugawaji wake kwa wachimbaji wadogo;
- Kupitia, kuandaa, kuratibu na kusimamia Sera, Sheria, taratibu na miongozo mbalimbali za kusimamia shughuli za wachimbaji wadogo ili ziwasaidie kufanya shughuli zao kwa kuzingatia kanuni za afya, usalama na mazingira;
- Kuandaa, kuratibu na kusimamia mafunzo ya wachimbaji wadogo kuhusu sera, sheria, taratibu na teknolojia sahihi za utafutaji, uchimbahi na uchenjuaji wa madini zinaziozingatia utunzaji bora wa mazingira;
- Kuratibu na kuandaa mikakati ya kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini ili waweze kupata sifa za kukopesheka na taasisi za fedha; na
- Kuratibu na kushiriki maonesho ya madini ya ndani ya nchi na nje ya nchi kwa lengo la kuvutia wawekazaji wa ndani na nje watakaoleta teknolojia, mitaji na vifaa kwa ajili ya kuendeleza wachimbaji wadogo.

## SEHEMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

- kutoa maoni ya mapitio ya kisera na kisheria kuhusu usimamizi wa mazingira katika sekta ya madini kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Divisheni ya Mazingira) ikiwemo masuala ya mabadiliko ya tabianchi.
- Kusimamia utekelezaji wa sera ya madini ili kupunguza athari mbaya za mazingira
- Ushauri wa utekelezaji wa sera kuhusu ulinzi na usimamizi wa mazingira
- Kuwezesha ujumuishaji wa masuala ya mazingira katika Mipango ya Wizara
- Kufanya Tathmini ya Kimkakati ya Mazingira (SEA) kuhusu sera, sheria, kanuni, mipango, mikakati na programu za kisekta.
- Kusimamia utayarishaji na utekelezaji wa tathmini ya athari za mazingira katika Sekta ya Madini
- Kuratibu na kutekeleza uanzishwaji wa Hati Fungani (Rehabilitation Bond) kwa ajili ya kurejereshea mazingira katika maeneo ya uchimbaji mkubwa endapo makampuni makubwa hayatakuwa na uwezo wa kurejereshea masuala ya mazingira.

## SEHEMU YA USIMAMIZI WA USHIRIKISHWAJI WA WAZAWA KATIKA RASILIMALI MADINI NA UWAJIBIKAJI WA MAKAMPUNI KATIKA JAMII

- Kuratibu utafiti juu ya uwezo uliopo wa ndani katika kutoa bidhaa na huduma zinazohitajika na makampuni ya madini na kupendekeza hatua zinazofaa ili kuongeza uwezo wa ndani.
- Kukuza uwekezaji katika uzundaji na utengenezaji wa vifaa vitakavyotumika katika sekta ya madini kwa maendeleo ya viwanda.

- Kukuza uwezo wa madini ulioainishwa na utafiti wa kijiolojia wa tanzania ili kuvutia maendeleo ya viwanda vya ndani.
- Kukuza utengenezaji wa ndani wa malighafi na vifaa vinavyotumika katika sekta ya madini.
- Kuratibu uanzishwaji na matengenezo ya kanzidata ya bidhaa na huduma zinazoweza kupatikana ndani ya nchi kwa muda mfupi, wa kati na mrefu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya manunuzi ya ndani.
- Kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kazi na mipango ya urithi na makampuni ya madini
- Kufanya uhamasishaji wa Ushirikishwaji wa Watanzania na kuwajengea uwezo Kukuza uhusiano kati ya makampuni ya madini na serikali za mitaa juu ya utekelezaji wa mpango wa Ushirikishwaji wa Watanzania na uwajibikaji kwa jamii kwa ulioidhinishwa kwa kushirikiana na tume ya madini na mamlaka husika za serikali za mitaa.
- Kuchambua ripoti za utendaji juu ya mipango wa Ushirikishwaji wa Watanzania na CSR ambayo huwasilishwa na Tume na kushauri ipasavyo

## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MADINI

**Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 yaliyofanyika Mwaka 2017 yamewezesha kufanyika kwa mabadiliko katika usimamizi wa Sekta ya Madini ambapo;**

- Majukumu ya iliyokuwa Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) na baadhi ya majukumu ya Kamishna wa Madini yamehamishiwa Tume ya Madini.
- Kila Mkoa una Ofisi ya Afisa Madini Mkazi.
- Kila mgodi mkubwa na wa kati utakuwa na Afisa Mgodi Mkazi.

## TAASISI ZILIZOPO CHINI YA WIZARA YA MADINI

- Tume ya Madini
- Taasisi ya Jiologia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST)
- Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)
- Kituo cha Jimolojia Tanzania (TGC)
- Taasisi ya Kuhamasisha Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia (TEITI)

**Wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo:**
**Wizara ya Madini,**
**Mji wa Serikali - Mtumba,**
**S.L.P 422,**
**DODOMA,**

**Simu: +255 26230051,**
**Nukushi: +255 26 2322282**
**Barua Pepe: ps@madini.go.tz**
**Tovuti: www.madini.go.tz**